JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAARIFA KUHUSU MCC/MCA NA HATUA ILIYOFIKIWA NA TANZANIA KATIKA KUANDAA MIRADI YA KUWASILISHWA

Millennium Challenge Corporation (MCC) ni Shirika lililoanzishwa na Serikali ya Marekani mwaka 2004 kwa lengo la kusimamia Mfuko maalum (Millennium Challenge Account) ulioanzishwa na Serikali hiyo kama sehemu ya utekelezaji wa maamuzi ya "**Monetary Summit**" ya 2002.

2. Mfuko huo ambao umezilenga zaidi nchi masikini sana duniani, unayo **madhumuni** makuu ya kusaidia katika kuchochea na kuendeleza jitihada za nchi masikini duniani na hasa zile ambazo zimepania zenyewe kujenga uchumi imara na endelevu, kuongeza vipato vya wananchi wake na hivyo kuwa katika nafasi nzuri ya kuboresha maisha yao kupitia miradi mbalimbali itakayotekelezwa kupitia mfuko huu. Kazi ya kuandaa miradi ni jukumu la nchi inayohusika ili mradi tu miradi hiyo iendane na vigezo mbalimbali vilivyowekwa na Serikali ya Marekani.

3. Serikali ya Marekani imeweka **vigezo vikuu vitatu** yaani nchi ambazo zimeonyesha kwa dhati jitihada za kuleta maendeleo ndani ya nchi zao kwa:

- Kutawala kwa haki;
- Kuwekeza katika rasilimali watu; na
- Kufungua milango katika biashara na uchumi

4. Kwa msingi huu, Novemba 2005 Tanzania nayo ilipata heshima ya kuwa miongoni mwa nchi 23 zilizopitishwa chini ya vigezo hivi na hivyo kuwa miongoni mwa nchi zinazoweza kuandaa maombi rasmi ya kupatiwa fedha kwa ajili ya kukuza uchumi wake na kuondoa umasikini.

5. Pamoja na Tanzania kushinda kwa vigezo vilivyowekwa, bado ilionekana kuwa tatizo la rushwa lilihitaji kufanyiwa kazi zaidi na hasa kwa kuelewa kuwa huwezi kuwa na uchumi endelevu ndani ya mazingira ya rushwa.

Hivyo, Tanzania ilikubaliwa kuwa na "Threshold Program" sambamba na zoezi la kuandaa "Country Compact Proposal (CCP)". Mkataba unaohusika wenye thamani ya $ 11.15m kwa ajili ya Utawala Bora, ulisainiwa kati ya Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mkuu wa Shirika la MCC tarehe 17 Mei, 06 mjini Washington. Fedha za mkataba huu zinasimamiwa na USAID kwa kushirikiana na sekta zinazohusika. Shughuli za utekelezaji zimekwisha kuanza. Sheria, Polisi, Vyama visivyo vya kiserikali, Habari na Mamlaka ya Ununuzi na Uthibiti wa Umma ni miongoni mwa Taasisi zitakazohusika.

6. Ni muhimu nieleze pia kuwa pamoja na kukubaliwa kushikiri, nchi zinazoshindwa kuendelea kuheshimu misingi iliyoziwezesha kukubaliwa zinafutiwa fursa hiyo hadi hapo zitakapojirekebisha. Mfano ni Gambia ambayo ushiriki wake ulisitishwa tarehe 16 Juni, 06.

B: MAENDELEO KATIKA KUKAMILISHA CCP YA TANZANIA

7. Zoezi la kuandaa Country Compact Proposal (CCP) lilianza mwezi Februari 2006 kwa kuanzia na uteuzi wa Mratibu wa MCC Tanzania. Tayari mambo yafuatayo yamefanyika au yanaendelea kufanyika:

(a) Ofisi ya MCC-Tanzania imepatikana na shughuli za matengezo muhimu zitakamilika kabla ya 30/06/06. Ofisi hizo ziko katika jengo la Water Front.

(b) Yamekuwepo mawasiliano ya karibu sana kati ya ofisi ya Mratibu na Wataalam wa MCC-Washington. Kati ya Januari na Juni 2006, wataalam wa MCC-Washington waliitembelea Tanzania kikazi mara tatu. Ziara ya mwisho ilikuwa kati ya tarehe 6 hadi 15 Juni, 2006.

(c) Wajumbe wa Kamati Elekezi wameteuliwa na wamekwishafanya vikao vitatu hadi ilipofikia tarehe 17/06/06. Kikao cha mwisho kilifanyika tarehe 13 Juni, 06. Mwenyekiti wa Kamati Elekezi ni Katibu Mkuu Hazina.

(d) Kamati ya Wataalam wa Kamati Elekezi imeteuliwa na imekuwa ndio muhimili mkuu katika maandalizi CCP ya Tanzania.

(e) Kamati ya Wataalam imekwishakamilisha rasimu tatu za CCP ya Tanzania hadi ilipofikia tarehe 11 Juni, 06. Rasimu iliyotolewa tarehe 11 Juni, 06 imekwisha kupitiwa na wataalam wa MCC na kuitolea mapendekezo muhimu kwa lengo la kuiboresha kwa misingi ya MCC na hivyo kukamilishwa kama Rasimu ya Mwisho. Vilevile, kikao cha Steering Committee cha tarehe 13 Juni, 06 kilipitia maeneo yote yanayojengewa hoja, na kukubaliana na mapendekezo ya miradi pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

(f) Pande zote mbili yaani "Steering Committee" na Wataalam wa MCC zimekubaliana kuwa **Rasimu** iliyokamilishwa tarehe 11 Juni, 06 inatoa sura nzuri na hivyo kinachohitajika sasa ni kuikamilisha kwa ajili ya hatua nyingine. Hatua hizo ni pamoja na kikao cha baadhi ya wadau, kujadiliwa na kupitishwa rasmi na Kamati Elekezi na hatimaye Baraza la Mawaziri.

(g) Baada ya hapo na kulingana na ratiba iliyokubaliwa na pande zote, "Compact" yetu itawasilishwa MCC Washington mwishoni mwa Julai, 2006.

(h) Zoezi la uchambuzi wa kina kwa upande wa MCC linatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2006 ikiwa ni baada ya kupata ridhaa ya "Investment Committee" ya MCC ambayo itakaa mwezi Agosti, 2006 kupitia "Opportunity Memorandum" itakayoandaliwa na MCC "Tanzania Transaction Team".

(i) Ni maoni ya Tanzania Transaction Team kuwa mchakato wa kina wa Compact yetu utaweza kukamilika mwakani na hivyo kuweza **kusaini** "Compact Package" ya Tanzania Mei, 2007.

(j) Kuhusu kiasi cha fedha kinachotarajiwa, maelekezo ya MCC-Washington yaliyopo ni kuwa tusizidi $ 800 kwa kipindi chote cha miaka mitano. Kama hali itaruhusu inawezekana kuwa na compact nyingine.

C. BAADHI YA MAMBO MUHIMU

8. Pamoja na maendeleo mazuri yaliyofikiwa katika kuandaa Compact Proposal ya Tanzania, bado safari ndiyo kwanza inaanza. Zoezi lililoko mbele yetu bado ni gumu na litahitaji mpangilio **mahiri** wa utendaji baina ya Idara mbalimbali za Serikali. Kanuni na taratibu zetu zinatakiwa ziwe wazi. Hakuna nafasi ya kubahatisha katika hatua zote kuanzia maandalizi ya Compact, uchambuzi wa awali na katika hatua ya utekelezaji. Pamoja na hayo, mambo yafuatayo ni muhimu:

(a) **Miradi inayopendekezwa**

Kulingana na upana wa mashauriano yaliyofanyika wakati wa kuandaa mpango wa Taifa wa kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini yaani MKUKUTA kwa Bara; na MKUZA kwa Zanzibar, zoezi la kupata miradi yenye kipaumbele halikuwa na tatizo. Tatizo limekuwa ni katika uwepo wa miradi mingi mno ukilinganisha na mategemeo ya fedha zinazotarajiwa kupatikana yaani kati ya $ 700 na $ 800 za kutumika ndani ya kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe ya kusainiwa kwa Compact yetu. Orodha ya miradi yote iliyokuwa imependekezwa na Timu ya Wataalam inayofikia $ 2221m imeambatanishwa kwa taarifa.

(b) Vigezo muhimu kwa miradi inayopendekezwa:

Kigezo cha msingi kwa miradi tunayoipendekeza ni kuwa na miradi yenye sifa za kuchochea ukuaji wa uchumi, uboreshaji endelevu wa mapato ya wananchi katika ujumla wao na hivyo kuboreka kwa hali ya maisha yao kwa kuimarisha njia za usafiri na usafirishaji na pia uwepo wa miundombinu bora ya upatikanaji wa nishati na maji.

Ni kutokana na lengo hili kuu, miradi iliyopendekezwa imeelekezwa kwenye:

- Upanuzi na uimarishaji wa miundombinu ya usafirishaji ili kuchochea ukuaji na uimarishaji wa shughuli za utalii na maendeleo ya kilimo Bara na Visiwani;
- Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa maji yenye uhakika kwa baadhi ya maeneo nchini kwa ajili ya matumizi ya majumbani na shughuli nyingine zile za kiuchumi mijini na vijijini;
- Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji na usambazaji wa nishati mijini na vijijini.

Kama ilivyoelezwa awali, upatikanaji wa miradi inayojibu hoja ya kukuza uchumi na kuondoa umasikini halikuwa tatizo. Miradi iliyopo ni mingi na imesambaa nchi nzima. Hivyo ili kupata orodha ya miradi ya kupendekezwa ilibidi kuwe na vigezo kadhaa vya kusaidia kupata uamuzi wa kuanzia hata kama havikuwa timilifu. Vigezo hivyo ni pamoja na:

(i) Miradi inayopendekezwa ni muhimu iwe na upembuzi yakinifu au angalau ule wa awali. Maandiko hayo yasiwe ya miaka mingi iliyopita;
(ii) Miradi inayopendekezwa ni lazima iwe na uwiano wa karibu sana na ukuaji wa uchumi na uondoaji wa umasikini na pia iwe na vigezo vinavyopimika;
(iii) Miradi inayopendekezwa iwe na uwiano na sekta nyingine zinazojibu hoja za ukuaji wa uchumi na uondoaji wa umasikini;
(iv) Miradi inayopendekezwa iwe ni sehemu ya miradi iliyoainishwa kwenye "Sectoral Master Plans" au "Sectoral Investment Programmes";
(v) Miradi inayopendekezwa iwe na idadi kubwa ya walengwa kwa misingi ya kiasi cha fedha kitakachotumika;
(vi) Kila mradi unaopendekezwa ni lazima uwe unatekelezeka na kukamilika katika kipindi kisichozidi miaka mitano;
(vii) Kila mradi unaopendekezwa uwe umejengewa mazingira ya kuwa endelevu (sustainable). Usiwe ni mradi tegemezi bali wenye uwezo wa kujiendesha kigharama. Uwe na uhalali kiuchumi; na
(viii) Mradi unaopendekezwa usiwe chimbuko la mgongano kati ya wafadhili.

(c) Ushirikishwaji wa Wadau

Suala hili lilijadiliwa na MCC baada tu ya Tanzania kukubaliwa kushiriki. Pande zote mbili zilikubaliana kuwa tofauti na nchi nyingine, hatuhitaji kuanza zoezi la ushirikishwaji upya. Kazi kubwa ilishafayika wakati wa mchakato wa MKUKUTA na MKUZA. Hata hivyo, ilikubaliwa kuwa itabidi vifanyike vikao vichache vya kutoa taarifa kwa baadhi ya wadau. Hadi sasa hivi yafuatayo yamefanyika kama sehemu ya muendelezo wa ushirikishwaji:

(i) Kamati Elekezi iliyoteuliwa ina wajumbe sio tu kutoka Serikalini bali hata kutoka nje ya Serikali. Hadi ilipofikia tarehe 15 Juni, 06, Kamati Elekezi ilikuwa na wajumbe wafuatao:

1. Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Mwenyekiti
2. Katibu Mkuu Wizara ya Mipango
3. Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini
4. Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu
5. Katibu Mkuu Wizara ya Maji
6. Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu
7. Katibu Mkuu TAMISEMI
8. Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje
9. Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar
10. Executive Secretary - Tanzania Business Council (TNBC)
11. Chief Executive Officer – (CTI)
12. Chief Executive Officer – TCCIA
13. Executive Director – TANGO
14. Technoserve/Tanzania International – NGO

(ii) Kamati ya Wataalam

Uteuzi wa Kamati ya Wataalam umezingatia muundo wa Kamati Elekezi. Lengo kuu ni kuona kuwa Compact ya Tanzania inakuwa ni matokeo ya ushirikishwaji ulio mpana zaidi. Kamati ya Wataalam imewashirikisha pia wataalam kutoka REPOA na ESRF katika maandalizi ya compact ya Tanzania.

(iii) Vikao na Donors

Jitihada za makusudi zimefanyka kuona kuwa "Lead Donors" wa kila sekta wanashirikishwa na Wizara husika. Hii ni kwa kuzingatia kuwa MCC haiji kama mshindani bali mshiriki katika kusaidiana na wengine katika kuleta maendeleo.

(iv) Kikao na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje

Tarehe 24 Machi,06 Mratibu wa MCC – Tanzania alitoa mada mbele ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje. Waheshimiwa Wabunge walikubaliana na mpango wa Serikali ya Marekani kuzisaidia nchi zinazoendelea na pia walikubaliana na sekta zilizopewa kipaumbele na Serikali yaani Usafirishaji, Maji na Nishati. Umwagiliaji ni sehemu ya maji.

(v) Mipango Mingine ya Ushirikishwaji

Maadam sasa tuko katika hatua ya ukamilishaji wa "Country Compact Proposal", ni nia ya "Steering Committee" kuwa vifanyike vikao vichache vya kutoa taarifa kuhusu hatua tuliyofikia katika maandalizi ya zoezi zima. **Ni baada ya hapo, Serikali itaombwa kutoa ridhaa yake kulingana na taratibu**. Katika hili, baadhi ya walengwa muhimu ni pamoja na:

- Kamati ya Fedha ya Bunge
- Kamati ya Huduma za Jamii ya Bunge
- Wanachama wa TANGO
- Wanachama wa CTI
- Wanachama wa TCCIA
- Wanachama wa TNBC
- Waandishi wa Habari

(d) Zoezi la "Due Diligence"

Baada ya MCC kupokea CCP yetu, hatua itakayofuata ni uandaaji wa kinachojulikana kama "Opportunity Memorandum". Hii itajadiliwa na "Investment Committee" ya MCC na baada ya kupitishwa kutolewa kibali rasmi kuitaka "**Tanzania Transaction Team"** kuanza zoezi la "Due – Diligence". Hatua hii ni muhimu sana kwani ndiyo itakayoainisha miradi inayostahili kupendekezwa

kuwasilishwa mbele ya **Bodi ya Wakurugenzi ya MCC.** Ni kwa msingi huo, miradi inayopendekezwa inatakiwa isiwe yenye mapungufu kimaandalizi. Inatakiwa iwe ni miradi iliyochambuliwa vema kiutaalam na ikapata ustahilifu (both economic and social) usioyumba. Miradi itakayoshindwa kivigezo, hata fedha zilizopendekezwa zitapotea na kuwa hasara kwetu. Miradi isiyo na upembuzi yakinifu na ambayo haitarajiwi kuikamilisha hatua hii ndani ya muda mfupi ni vema isijumuishwe ingawa wengi tungependa iwepo. Vinginevyo, inaweza pia ikawa ni chanzo cha kuchelewesha maamuzi ya MCC.

E. MWISHO

9. Maelezo haya yametolewa ili kutoa nafasi ya suala la MCC/MCA kueleweka vizuri zaidi. Kazi ya kukuza uchumi na kuondoa umasikini sio kazi ya Serikali pekee. Ni kazi inayohitaji ushirikiano wa karibu sana kati ya watendaji wa Serikali na wananchi kwa ujumla. Wakati kazi kubwa ya Serikali ni kuboresha mazingira, kazi ya wananchi na wawekezaji ni kuyatumia mazingira hayo kwa kufanya kazi kwa ubunifu, bidii, kujituma na kuacha kulalamika. Wakati huo huo watumishi wa Serikali nao wanatakiwa kufanya kazi kwa haki, bidii, uaminifu, uadilifu na usikivu yakinifu. Hakuna njia ya mkato ya kukuza uchumi na kuondoa umasikini.

Imetolewa na Ofisi ya:
Mratibu wa MCC-TANZANIA
2 Julai, 2006